

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA**



**MKATABA MDOGO WA UJENZI WA JENGO
LA WAGONJWA MAHUTUTI**

KATIKA

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SONGWE

NOVEMBA, 2021

MKATABA WA UJENZI

MKATABA WA KUJENGA JENGO LA WAGONJWA MAHUTUTI (ICU)

Mkataba huu umefungwa kati ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe S.L.P. 301, Songwe (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama mwajiri) kwa upande mmoja

NA

HASSAN IDDI IDDIWA SLP... SONGWE ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Fundi Mkuu (Local fundi) kwa ajili ya kujenga **JENGO LA WAGONJWA MAHUTUTI (ICU)**.

Fundi mkuu (Local fundi) atafanya kazi ya kujenga **JENGO LA WAGONJWA MAHUTUTI (ICU)** kwa thamani ya shilingi Millionsi Themanini Mia Tisa Sabini na Nne elfu Mia mbili Sitini na Tisatu. **(TSHS. 80,974,269.00)**.

1.0 TAFASIRI

Makubaliano haya yamefanyika na kushuhudiwa kama ifuatavyo:-

1.1 Fundi mkuu (Local Fundi) maana yake ni mtu aliyeingia mkataba na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe kwa ajili ya kujengajengo la **Wagonjwa Mahututi (ICU)**.

1.2 Hospitali maana yake ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe.

2.0 Utoaji wa huduma hii

Fundi mkuu/ Local fundi atafanya kazi ya kujenga jengo la Wagonjwa Mahututi (ICU).

2.1 Pale patakapokuwa na hitaji maalumu kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe na sio vinginevyo.

2.2 Fundi mkuu/Local fundi atatakiwa kufanya kazi hiyo ndani ya muda wa **miezi mitatu na wiki tatu ambayo itakamilika tarehe 15 Juni. 2022.**

2.3 Iwapo Fundi mkuu/Local fundi atachelewa kuanza na kumaliza kazi hiyo kama inavyotakiwa katika mkataba huu, mwajiri atakuwa na mamlaka ya kuvunja mkataba huu na kuajiri Fundi mkuu/Local fundi mwingine.

3.0 MALIPO.

3.1 Mkandarasi/Fundi atalipwa kwa hatua zifuatazokadri anavyoendelea na ujenzi na baada ya mwajiri kukagua na kuridhika na jengo husika.

- A. Ujenzi wa kuta za msingi.
- B. Zege la jamvi, Nguzo za awali na Mkanda wa chini (Ground beam).
- C. Ujenzi wa Boma na mguzo
- D. Ring beams, linterna kuta baada ya ring beams.
- E. Kuezeka / Kupaua.
- F. Plasta na Floor screed

- F. Plasta na Floor screed
- G. Ngazi na Ngazi mtelezo.
- H. Mifumo ya awali ya maji safi-na maji taka (ndani ya jengo) na mifumo ya awali ya umeme.
- I. Marumaru za kuta na sakafu
- J. Brandering na kufunga gypsum boards
- K. Skimming na Rangi.
- L. Wayaring ya umeme na mfumo wa zima moto
- M. Mfumo wa maji safi na maji taka (nje ya jengo) na ujenzi wa mashimo ya vyoo.
- N. Usafi kuzunguka jengo na kuondoa mabaki ya vifaa.

- 3.2 Malipo yatakuwa kwa hundi/Benki baada ya Fundi mkuu/ Local Fundi kuwasilisha madai na kwa kuzingatia aya ya 3.1 ya mkataba huu.
- 3.3 Fedha ya zuio (Retention money) itakua asilimia 5 (5%) ya malipo na itakatwa kuanzia hati ya malipo namba mbili na italipwa baada ya kipindi cha matazamio ya uharibifu kukamilika.

4.0 MUDA WA MKATABA NA TATHIMINI YA MKATABA.

- 4.1 Mkataba huu ni wa kipindi cha Miezi mitatu na wiki tatu
- 4.2. Mkataba unaweza kufanyiwa tathimini na mapitio kwa niaba ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe ili kujiridhisha na kiwango na ubora wa utendaji kazi wa Fundi mkuu/Local fundi.
- 4.3 kipindi cha matazamio ya uharibifu (Defect liability period) kitakua miezi sita (6) tangu fundi mkuu kukabidhi kazi.

5.0 WAJIBU WA FUNDI MKUU/LOCAL FUNDI

- 5.1 Fundi mkuu/Local fundi anatakiwa kufanya kazi kama alivyoagizwa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe na kwa muda muafaka na katika ubora unaotakiwa.
- 5.2 Fundi mkuu/Local fundi hatoruhusiwa kutoa kazi hii kwa mtu mwingine au chombo chochote kingine bila kibali cha mwajiri (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe).
- 5.3 Fundi mkuu/Local fundi atawajibika kwa uharibifu wowote utakaosababishwa na uzembe wa watumishi wake au yeye mwenyewe wakati wa utekelezaji wa mkataba na hata baada ya kumalizika kwa mkataba.

6.0 WAJIBU WA MWAJIRI

- 6.1 Mwajiri atawajibika kuweka mazingira bora ya kumuwezesha Fundi mkuu/Local Fundi kufanya kazi yake kwa ufanisi.
- 6.2 Mwajiri atawajibika kumletea fundi vifaa vya ujenzi katika eneo la ujenzi kwa muda Muafaka.

7.0 MUDA WA MAKUBALIANO

- 7.1 Mkataba huu ni wa kipindi cha miezi minne tangu Fundi mkuu kukabidhiwa eneo la ujenzi na baada ya hapo mkataba mwingine unaweza kuwekwa kwa makubaliano ya pande zote mbili.

